JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

TAARIFA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2016

MKOA WA MTWARA

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
S.L.P 544
Simu: 023 2333014
Nukushi: 023 2333194
Barua pepe:rasmtwara@pmoralg.go.tz
Tovuti: www.mtwara.go.tz

1.0 UTANGULIZI

Uongozi na wananchi wa Mkoa wa Mtwara wanayo furaha kubwa kuupokea Mwenge wa Uhuru. Tunayo matumaini makubwa na mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016 hapa mkoani kwetu kwa kuwa tunatambua kazi kubwa inayofanywa na Mwenge tangu kuwashwa kwake mwaka 1961.

Ndugu Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Ndugu George Jackson Mbijima pamoja na wakimbiza Mwenge Kitaifa tunawakaribisha sana hapa Mkoani Mtwara, tunawapongeza kwa kupewa dhamana kubwa ya kuukimbiza Mwenge wetu wa Uhuru. Aidha tunawatakia kila la heri mmalize mbio hizi kwa usalama salmin.

2.0 ULINZI NA USALAMA

Hali ya ulinzi na usalama Mkoani ni shwari na inaendelea kuimarika. Matatizo yanayojitokeza yameendelea kudhibitiwa na Vyombo vya Dola kwa kushirikiana na raia wema.

3.0 UTAWALA NA MAKAZI

Mkoa wa Mtwara una eneo la kilometa za mraba 16,720. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi , Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Mkoa unakadiriwa kuwa na watu 1,340,300 (Wanaume 632,416 na Wanawake 6707,884), wastani wa ongezeko la watu nlikiwa ni asilimia 1.2 kwa mwaka.

Mkoa umegawanyika katika Wilaya 5, Halmashauri 9, Tarafa 27, Kata 149, Vijiji 694, Vitongoji 2,950 na Mitaa 244. Aidha tunayo Mamlaka (1) moja ya Mji midogo wa Mahuta.

4.0 HALI YA SIASA

Hali ya kisiasa Mkoani ni Shwari na tuna jumla ya vyama 11 vinavyofanya kazi za siasa. Aidha Mkoa una Majimbo ya Uchaguzi kumi (10) ambayo (Mtwara Mjini, Mtwara Vijijini, Nanyamba, Tandahimba, Newala Mjini, Newala Vijijini, Masasi, Ndanda, Lulindi na Nanyumbu).

MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2015/16

Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2015/16 zilizokuwa zimebeba Ujumbe usemao "***Tumia haki yako ya kidemokrasia"*** chini ya Kauli Mbiu "**Jiandikishe na kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka 2015",** Kupitia ujumbe huo Mkoa wetu wa Mtwara ulitekeleza vyema kwa kufanya zoezi la uandikishaji tarehe 24 Aprili, 2015 ambapo utekelezaji ulikuwa ni asilimia 98.9.

Sambamba na ujumbe huu, Mkoa wa Mtwaara ulitekeleza kikamilifu ujumbe wa kudumu juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI, Rushwa, na matumizi ya dawa za kulevya kama ifuatavyo:

- ***Kata minyororo ya Rushwa***; chini ya kauli mbiu **Chagua kiongozi Mzalendo**

  Mkoa wa Mtwara umekuwa ukianzisha vilabu vya wapinga rushwa mashuleni na kusambaza machapisho kwa wananchi kwa lengo la kuwajengea ufahamu kuhusu tatizo la rushwa, madhara yake na kuongeza ari ya kupambana na tatizo hilo kupitia mbinu shirikishi. Aidha mikutano ya uhamasishaji inaendelea kufanyika katika maeneo ya Wilaya zote.

- ***Uteja wa dawa za kulevya unazuilika na Kutibika***; chini ya kauli mbiu **Chukua hatua**

  Mapambano dhidi ya matumizi ya dawa za kulevya yanaendelea na tangu kupita kwa Mwenge wa Uhuru. Wananchi hasa vijana wameendelea kuelezwa athari za dawa za kulevya na kwa waatirika wa dawa hizo wamekuwa wakisaidiwa kuachana nazo kupitia programu maalum inayotekelezwa na Hospitali ya Ligula kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na raia wema wameendelea kupambana na wote wanaojihusisha na matumizi ya dawa za kulevya au uingizaji na uuzaji wa dawa hizo.

- ***Vijana wa leo na UKIMWI;*** chini ya kauli mbiu **Wazazi tuwajibike**

  Mapambano dhidi ya Maambukizi mapya ya UKIMWI yanaendelea ambapo semina mbalimbali juu ya VVU/UKIMWI zimeendelea kutolewa na upimaji wa hiari umeendelea kuongezeka kwa makundi mbalimbali ya kijamii.

- ***Wekeza katika maisha ya badae***; chini ya kauli mbiu **Tokomeza malaria**

  Mapambano dhidi ya Malaria yanaendelea, jamii imeelimishwa juu ya usimamiaji wa usafi wa mazingira. Aidha zoezi la ugawaji wa vyandarua kwa wananchi linaendelea, na hadi sasa Zaidi ya Vyandarua 525,488 vimeshagawiwa kwa wananchi na maambukizi ya Malaria yamepungua toka 33.6% mwaka 2010/11 hadi 17% mwaka huu.Tarehe 28 Mei, 2016 Mkoa umezindua awamu mpya ya ugawaji wa vyandarua kwa wamama wajawazito na watoto chini yam waka mmoja ikiwa ni muendelezo wa mapambano hayo.

MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2016/2017

Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2016/2017 zimeanza rasmi leo tarehe 31 Mei 2016 katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani na kutarajiwa kukamilika tarehe 06 Juni, 2016 katika Wilaya ya Nanyumbu. Mbio hizo zitakimbizwa kwa siku sita zikipita katika Wilaya zote tano za Mkoa wetu na Halmashauri zake.

Mbio hizi zimebeba ujumbe uisemayo "***Vijana ni nguvu kazi ya Taifa: Washirikishwe na kuwezeshwa",*** ujumbe ambao Mkoa wetu wa Mtwara unatekeleza vyema ambapo Halmashauri, Wizara yenye dhamana na Vijana na wadau mbalimbali wa maendeleo

Mkoa wa Mtwara umeendelea kuwawezesha vijana katika nyanja mbalimbali kama ambavyo Mbio hizi zitashuhudia na kupokea taarifa kupitia miradi mbalimbali. Mkoa kupitia Halmashauri zake umeendelea kutoa mikopo kwa vijana na wanawake ambapo kwa bajeti ya 2015/16 utekelezaji umefikia 82% na ifikapo tarehe 30 Juni, 2016, tutakuwa tumetekeleza lengo la 5% kwa vijana na 5% kwa wanawake kwa 100% kama ilivyoagizwa na Serikali.

Sambamba na ujumbe huu, kuna ujumbe wa kudumu juu ya mapambano dhidi ya UKIMWI, Rushwa, na matumizi ya dawa za kulevya ulivyoainishwa kama ifuatavyo:

- ***Timiza wajibu wako:*** chini ya kauli mbiu ***Kata minyororo ya rushwa.***
- ***Tujenge Jami, Maisha na Utu Wetu:*** chini ya kauli mbiu ***Bila dawa za kulevya***
- ***Tanzania bila maambukizi mapya, Unyanyapaa na vifo vitokanavyo na UKIMWI:*** chini ya kauli mbiu ***Inawezekana***
- ***Wekeza katika maisha ya badae***; chini ya kauli mbiu **Tokomeza malaria**

Mkoa umejipanga vyema na unaendelea kupambana na mambo yote manne ikiwamo Rushwa, UKIMWI, Dawa za Kulevya na Malaria. Haya yatajionyesha wazi katika taarifa za Wilaya na miradi itakayopitiwa na Mwenge.

Mbio za Mwenge wa Uhuru zitakimbizwa kwenye umbali wa Km 662.9 (Nanyumbu km 172, Masasi km 101.2 Newala km 109 Tandahimba km 107.2 Mtwara Vijijini km 109 na Mtwara Manispaa km 64.5) kukiwa na jumla ya Miradi 40 yenye thamani ya shilingi **49,821,075,268 (Bilioni arobaini na tisa milioni mia nane ishirini moja na elfu sabini na tano** kwa mchanganuo ufuatao:

• **Mchango wa Wananchi**	**shs. 1,864,460,134**	**(4%)**
• **Mchango wa Halmashauri**	**shs. 1,230,913,030**	**(3%)**
• **Mchango wa Serikali Kuu**	**shs. 31,041,469,955**	**(62%)**
• **Mchango wa Wahisani**	**shs. 15,684,232,149**	**(31%)**

Kati ya Miradi hiyo 40, miradi 8 itazinduliwa, miradi 5 itafunguliwa, 9 itawekwa jiwe la msingi na miradi 18 itakaguliwa.

Nirudie tena kumuomba Mwenyezi Mungu atujalie na kuukimbiza Mwenge wa Uhuru mwaka 2016, kwa Amani na utulivu.

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2016 HALMASHAURI YA MANISPAA YA MTWARA MIKINDANI.

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI(KM)	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
31/5/2016	12.00 – 3.00	Mpapura	0	Kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Mkoa wa Mtwara	Wananchi wote
	3.00 – 3.15	Mpapura	26	Msara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mikindani	
	3.15 – 5.15	Mikindani	00	• Kuweka Jiwe la Msingi Uendelezaji wa Mji Mkongwe wa Mikindani • Kukagua Majengo ya Kale • **UJUMBE WA MWENGE** • Kuona na Kukagua Shughuli za Mafunzo ya Uhotelia Kwa Vijana • Kuona na Kukagua shughuli za Ujasiriamali za Vijana na Kukabidhi toa Hundi kwa Vijana na Wanawake • Chai	DC
	5.15 – 5.20	Mikindani	2	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mitengo	DC
	5.20 - 5.45	Mitengo	0	Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa Hospitali ya Rufaa	DC
	5.45 - 6.00	Mitengo	12.5	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kulekea Chuno kupitia Magomeni	DC
	6.00 - 6.25	Chuno	00	• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la uzinduzi wa barabara ya Chuno	DC
	6.25 - 6.35	Chuno	6.2	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelkea Shangani kupitia Mangowela	DC
	6.35-7.00	Shangani	00	• Kukimbiza Mwenge • Kuwekajiwe la msingi ujenzi wa vyumba 3 vya maabara shule ya sekondari Shangani	DC
	7.0 0- 7.10	Shangani	4	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Coco Beach kupitia Indian Ocean	DC
	7.10 - 9.10	Coco Beach	00	• Kukimbiza Mwenge • Taarifa ya wajasiliamali • Kuona na kukagua shughuli za wajasiliamali vijana na wanawake na kutoa hundi • **UJUMBE WA MWENGE** • Chakula cha mchana	DC
	9.10 - 9.20	Coco Beach	4	Msafara wa Mwenge wa Uhru kulekea Vigaeni kupitia Bandari Road na Raha Leo	DC
	9.20 - 9.30	Vigaeni	00	• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua ujenzi wa Benki Kuu	DC
	9.30 - 9.35	Vigaeni	3	Msafara wa Mwenge wa Uhru kulekea Ofisi ya Madini Kanda ya Kusini	DC
	9.35 - 9.40	Rahaleo	00	• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua ujenzi wa Ofisi ya Madini Kanda ya Kusini	DC
		Rahaleo	00	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kulekea Uwanja wa Mashujaa	
	9.40 -10.45	Mashujaa		• Kuona na kukagua banda la mapambano dhidi ya Malaria, rushwa, dawa za kulevya na VVU/UKIMWI • **RISALA YA UTII** • **UJUMBE WA MWENGE** • **Mkesha**	DC
01/06/2016	Chikongola	1.00 – 2.30	0	CHAI	DC
	Kitope	2.30 – 3.00	10.9	Kukabidhi Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	DC

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2016 HALMASHAURI YA WILAYA MTWARA.

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI (KM)	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
01/6/2016	3.00 – 3.40	Kitope – Naumbu	0	Kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani	Wananchi wote
	3.40 – 4.30	Naumbu		Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Kijiji cha Imekuwa	
	4.00 – 4.15	Imekuwa	5	• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa kituo cha maarifa ya kilimo na mifugo Kata ya Naumbu. • Kusalimia wananchi	DC
	4.15 – 5.40	Imekuwa	26	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mkunwa kupita vijiji vya Hiari, Nangumi, na Likonde	DC
	4.40 – 5.40	Mkunwa	00	• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua shughuli za ujasiriamali za vikundi vya vijana, wanawake na walemavu • **UJUMBE WA MWENGE** • Chai ya Asubuhi	DC
	5.40 –6.55	Mkunwa	34	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mnima kupitia vijiji vya Mporondomo, Namanjele, Mangopachanne, Ilala, na Mtama	DC
	6.55 – 7.55	Mnima	00	• Kukimbiza Mwenge • **UJUMBE WA MWENGE** • Chakula cha mchana	DC
	7.55-9.40	Mnima	33	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Dinyecha kupitia vijiji vya Namambi, Njengwa, Mtuli – Njengwa, Mtuli – Hinju, Kitachi, Hinju, Mibobo na Migombani	DC
	9.40 – 10.10	Dinyecha	00	• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa barabara ya lami km 1.6 • Kusalimia wananchi	DC
	10.10 – 10.30	Dinyecha	3	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kulekea Nanyamba	
	10.30 – 12.00	Nanyamba		• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua banda la mapambano dhidi ya Malaria, rushwa, dawa za kulevya na VVU/UKIMWI • **RISALA YA UTII** • **UJUMBE WA MWENGE** • Mkesha	DC
02/06/2016	1.00 – 2.00	Nanyamba	00	Chai ya Asubuhi	DC
	2.00 – 2.15	Nanyamba	8	Mwenge kulekea Miuta	DC
	2.15 – 2.25	Miuta		Kukabidhi Mwenge wa Uhuru Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba	DC

RATIBA YA NJIA YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2016 WILAYA YA TANDAHIMBA

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI (KM)	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
02/06/2016	2.25 - 4.00	Miuta	0	Kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara	Wananchi wote
	4.00-4.20	Matende	21.6	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mwangaza kupitia kijiji cha Matende	DC
	4.20-4.30	Mwangaza	00	• Kukimbiza Mwenge • Kukagua na kukabidhi madawati 4000 kwa ajili ya shule zenye upungufu	DC
	4.30-4.35	Mtikula	3	Mwenge utapita polepole ukiwa kwenye gari	DC
	4.35-5.50	Namikupa	6	• Kukimbiza Mwenge • Kufungua chumba cha upasuaji Kituo cha AFya Namikuapa • **UJUMBE WA MWENGE** • Chai ya asubuhi	DC
	5.50-6.10	Tandahimba	6	• Kukimbiza Mwenge • Kuzidnua nyumba 6 za wakuu wa vitengo	DC
	6.10-6.40	Malamba	6.4	Mwenge kuelekea Nahyanga kupitia vijiji vya Miule, na Mnaida,	DC
	6.40-7.00	Nanhyanga	10.2	• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la msingi vyumba 3 vya maabara shule ya sekondari Nanhyanga • **UJUMBE WA MWENGE**	DC
	7.00-8.00	Nanhyanga	3.3	Chakula cha mchana	DC
	8.00-8.30	Mnaida	3.1	Mwenge kuselekea Tandahimba kupitia vijiji vya Miule, na Malamba	DC
	8.30-9.00	Tandahimba	7.2	• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la msingi kiwanda cha ubanguaji korosho cha AMAMA Farms Tandahimba	DC
	9.00 – 10.00	Tandahimba eneo la kuegesha magari	3.9	• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua shughuli za ujasiriamali za vijana na wanawake na kutoa Hundi kwa vikundi 2 vya mfano vya Amani (vijana) na Amkeni (wanawake)	DC
	10.00 – 12.00	Matogoro	4.7	• Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua banda la mapambano dhidi ya Malaria Ugawaji wa vyandarua), rushwa, dawa za kulevya na VVU/UKIMWI (zoezi la upimaji wa VVU/UKIMWI kwa hiari) • **Risala ya Utii** • **UJUMBE WA MWENGE** • Mkesha	DC
03/06/2016	1.00-1.45	Tandahimba	0	Chai	DC
	1.45 – 2.00	Tandahimba	26	Mwenge kulekea Lidumbe Shule	DC
	2.00 – 2.30	Lidumbe Shule		Makabidhiano	DC

RATIBA YA NJIA YA MWENGE WA UHURU MWAKA 2016 WILAYA YA NEWALA

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI (KM)	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
03/06/2016	2.30 – 3.30	Lidumbe shuleni	00	Kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Wilaya ya Tandahimba	Wananchi wote wa Wilaya ya Newala
	3.30 – 4.00	Lidumbe Shuleni	14	Msafara wa Mwenge wa uhuru kuelekea Makondeko kupitia vijiji vya Mahumbika na Chikwaya	DC
	4.00 - 4.15	Makondeko	4	• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa nyumba ya walimu 6 kwa 1 Shule ya sekondari Makote	DC
	4.15- 5.30	Makondeko	8	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mkunya kpitia kijiji cha Kiuta	DC
	4.30 – 5.30	Mkunya	00	• Kukimbiza Mwenge • Kuweka jiwe la msingi Kituo cha afya Mkunya • **UJUMBE WA MWENGE** • Chai ya asubuhi	DC
	5.30 -6.40	Mkunya	19	Mwenge kulekea Newala Mjini kupitia vijiji vya Magumchila, Nanguruwe, Mnanje na Kilimahewa	DC
	6.45 - 9.00	Newala Mjini	4	• Kukimbiza Mwenge • Kuzindua barabara ya lami Km1 Newala Mjini • Kuona na kukagua shughuli za vijana katika kujiletea maendeleo • Kuona na kukagua shughuli za ujasiriamali za wanawake • **UJUMBE WA MWENGE** • Chakula cha mchana	DC
	9.00 – 9.30	Amkeni	3	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Mtangalanga kupitia vijiji vya Amkeni na Mnuvii	DC
	9.30 – 9.45	Mtangalanga	4	• Kukimbiza Mwenge • Kufungua Hosteli ya wakulima Kituo cha Maarifa ya Kilimo Mtangalanga	
	9.45 – 12.00	Mtangalanga	4	• Kukimbiza Mwenge • Kupata taarifa ya Wilaya kuhusu juhudi za kupambana na VVU/UKIMWI, dawa za kulevya, malaria na rushwa (kuzindua klabu ya wapinga rushwa shule ya msingi Mtangalanga) • **RISALA YA UTII** • **UJUMBE WA MWENGE** • Mkesha wa Mwenge	DC
04/06/2016	12.00-1.00	Mtangalanga	0	CHAI	DC
	1.00 - 2.45	Mtangalanga	55	Mwenge kulekea Ndanda	DC
	2.45 – 3.30	Ndanda	0	Mwenge utapita polepole ukiwa ndani ya gari	DC

RATIBA YA MWENGE WA UHURU WILAYA YA MASASI TAREHE 04/06/2016

TAREHE	MUDA	MAHALI	KM	TUKIO/SHUGHULI	MHUSIKA
05/06/2016	3.30 – 4. 00	**NDANDA**	00	Uongozi wa Wilaya ya Masasi kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa Uongozi wa Wilaya ya Newala	DC
	4.00 – 5. 30	Ndanda	00	• Kupokea taarifa ya Mradi naKuzindua mradi wa ufugaji wa Kuku wa nyama na Mayai Ndanda Sekondari • Kuona na kukagua shughuli za utengenezaji wa Madawati • **UJUMBE WA MWENGE** • **CHAI – Zakeo Ndanda**	DC
	5. 30- 6.00	Mwena	3	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kulekea Mena • Kupokea taarifa ya Mradi na Kuweka Jiwe la Msingi kiwanda cha kutengeneza chupa za Maji na vifungashio vya bidhaa mbalimbali	DC
	6.00 – 6.30	Mwena	24	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea Chikukwe kupitia vijiji vya Chikundi na Chigugu	DC
	6.30 – 7. 00	Chikukwe		• Kupokea taarifa ya mradi • Kuona na kukagua Shamba la Muhogo aina ya Kiroba	DC
	7.00 – 7. 15	Chikukwe	20	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kulekea Shule ya Msingi Mkuti kupitia kijiji cha Maili Sita	DC
	7.15 – 9. 15	S/Msingi Mkuti	00	• Mwenge utakimbizwa Kupokea taarifa ya vikundi vya ujasiriamali • Kuona na kukagua vibanda vya vikundi vya vijana na wanawake • **Kukabidhi HUNDI ZA MIKOPO** • **UJUMBE WA MWENGE** • **CHAKULA**	DC
	9.15– 9. 30	Mkomaindo	3.2	• Kupokea taarifa ya mradi • Kuzindua Barabara ya Lami kutoka Rest camp hadi TK km 1.15	DC
	9. 30	Napupa	1	• Mwenge utakimbizwa • Kutembelea, kukagua na kupata taarifa ya Mabanda mbalimbali ya Maonyesho • **RISALA YA UTII** • Utambulisho wa Viongozi na Wakimbiza Mwenge kitaifa • **UJUMBE WA MWENGE** • **MKESHA WA MWENGE**	DC
03/06/2016	12.00 – 1.00	Eneo la Ikulu	00	**CHAI YA ASUBUHI**	DC
	1.00 – 3.10	Eneo la Ikulu	50	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kulekea Horora	DC
	3.10 – 3.30	**Horora**	0	Uongozi wa Wilaya ya Masasi kukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa Uongozi wa Wilaya ya Nanyumbu	DC

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MWAKA 2016 WILAYA YA NANYUMBU

TAREHE	MUDA	MAHALI	UMBALI KM	SHUGHULI/TUKIO	MHUSIKA
5/6/2016	2.00 - 3.00	Horora	0	Kupokea Mwenge wa Uhuru kutoka Wilaya ya Masasi	DC
	3.00 – 3.45	Horora	0	• Mwenge kukimbizwa • Kuweka jiwe la msingi ujenzi wa nyumba ya walimu 6 kwa 1 shule ya sekondari Maratani • **UJUMBE WA MWENGE**	DC
	3.45 – 4.00	Horora	38	Mwenge kuelekea Nangomba kupitia vijiji vya Mnanje A, Chikunja II, Namatumbusi, Kilosa, Mikangaula, Lowasa, Nahimba,	DC
	4.00 – 4.30	Nangomba	0	• Kukimbiza Mwenge • Kuzindua kituo cha mafuta Nangomba	DC
	4.30 – 4.35	Nangomba	0	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea eneo la CHAI	DC
	4.35 – 5.00	Nangomba	0.200	CHAI	DC
	5.00 – 6.05	Nangomba		Mwenge wa Uhuru kulekea Nanyumbu kupitia vijiji vya Mnemeka na Chitowe	DC
	6.05 – 6.30	Nanyumbu		Mwenge wa Uhuru kuwasilili Nanyumbu • Kukimbiza Mwenge • Kufungua mradi wa Ghala la Mazao • Kuzindua Ghala	DC
	3.30 – 7.30	Nanyumbu	65	Msafara wa Mwenge Kuelekea Mara kupitia vijiji vya Maneme, Namasongo, Chipuputa, Mkohora, Nahawa, na Mangaka	DC
	7.30 – 7.50	Mara - Sengenya	0	Msafara wa Mwenge wa Uhuru Kuwasili Mara - Sengenya • Kukimbiza Mwenge • Kufungua miradi ya Ujasiliamali ya vijana na wananwake • **UJUMBE WA MWENGE**	DC
	7.50 – 8.00	Mara - Sengenya	0.200	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuelekea kwenye mradi wa Ujasiliamali wa Vijana na Wanawake Sengenya	DC
	8.00 – 8.30	Sengenya	0	• Kukimbiza Mwenge • Kukagua miradi ya Vijana na Wanawake • **UJUMBE WA MWENGE**	
	8.30 – 9.30.	Sengenya	0	CHAKULA CHA MCHANA	DC/WOTE
	9.30 – 9.40	Sengenya	2	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kulekea Mangaka	DC
		Mangaka	0	Msafara wa Mwenge wa Uhuru kuwasili uwanja wa Mkeshai • Kukimbiza Mwenge • Kuona na kukagua mabanda ya TAKUKURU, Afya, VVU/UKIMWI, Malaria na dawa za kulevya • **Risala ya Utii** • **UJUMBE WA MWENGE NA Mkesha**	DC
6/6/2016		Mangaka	0	Chai	DC
		Mangaka	59	Msafara wa Mwenge kuanza safari kuelekea Chivirikiti	DC
	2.40-3.45	Sautimoja	0	Uongozi wa Wilaya ya Nanyumbu kukabidhi Mwenge kwa Uongozi wa Mkoa wa Mtwara	DC

RATIBA YA MAKABIDHIANO YA MWENGE WA UHURU 2016
KATI YA MKOA WA MTWARA NA RUVUMA

TAREHE	MUDA	MAHALI	TUKIO	MHUSIKA
	2.40-2.45	Sautimoja	Uongozi wa Wilaya ya Nanyumbu kukabidhi Mwenge kwa Uongozi wa Mkoa wa Mtwara.	DC Mtwara, RC Mtwara
	2.45-2.50	Sautimoja	Kuwatambulisha Viongozi wa Chama na Serikali wa Mkoa wa Mtwara.	Mratibu wa Mwenge (M)
	2.50-2.55	Sautimoja	Salamu za Mkoa za kuwaaga Wakimbiza Mwenge Kitaifa	RC Mtwara
	2.55-3.00	Sautimoja	Kuwakabidhi Wakimbiza Mwenge Kitaifa kwa Uongozi wa Mkoa wa Ruvuma	RC Mtwara
	3.00-3.05	Sautimoja	Kuukabidhi Mwenge wa Uhuru kwa RC Ruvuma.	RC Mtwara Ruvuma

RATIBA YA MBIO ZA MWENGE WA UHURU MKOANI MTWARA
31 MEI – 6 JUNI, 2016

31/05/2016
Halmashauri ya Manispaa Mtwara Mikindani

01/06/2016
Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara Vijijini

02/06/2016
Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba

03/06/2016
Halmashauri ya Wilaya ya Newala

04/06/2016
Halmashauri ya Wilaya ya Masasi

05/06/2016
Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu

"VIJANA NI NGUVU KAZI YA TAIFA; WASHIRIKISHWE NA KUWEZESHWA"